



# 16

## Siku za Uanaharakati 2024

Uwajibikaji, Rasilimali, na Maazimio.

### Mwongozo Wa Shughuli Za Kampeni



## Utangulizi

Katika mwaka huu wa 2024, tunaungana sote kwa ajili ya kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati ili kusesitiza dhamira yetu inayotokana na azimio la Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing lenye Maono ya Kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake kwa kutenga rasilimali za kutosha, na kuwepo na mifumo ya uwajibikaji. Kiti ya utetezi na kuchukua hatua ya mwaka huu inajumuisha nyenzo kadhaa za kukusaidia katika shughuli zako za kampeni kama vile: Utepe wa Zambarau au Nyeupe, Nyaraka za Kampeni, Mabango, Kadi za Safina, Vijitabu, na nyenzo za kutengeneza Bangili za Urafiki. Shughuli zinaweza kufanywa katika ngazi ya mtu binafsi, shirika na jamii. Tafadhali jiunge nasi kufanya utetezi ili tuwe na dunia iliyo salama kwa wote, tunapotoa azimio kwa mara nyingine la kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake kwa kutenga rasilimali za kutosha, na kuwepo na mifumo ya uwajibikaji.

### 1. Fahamu vizuri kuhusu nyaraka za Kampeni

Kiti hii ina nyaraka muhimu zitakazo kusaidia kwenye maandalizi yako ya kampeni. Muhtasari wa Kampeni unatoa utangulizi wa kina, sababu na malengo yanayowiana na eneo muhimu lililo tolewa kwenye Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing linalohusu Ukatili Dhidi ya Wanawake. Mwongozo wa Shughuli za Kampeni unatoa shughuli zinazopendekezwa kwa watu binafsi, mashirika na jamii.





## 2. Andaa Majadiliano ya Bango la Kampeni

Bango la kampeni linaonyesha umuhimu wa uwajibikaji katika kushughulikia masuala ya Ukatili Dhidi ya Wanawake. Tumia bango ili kuchangamsha mazungumzo na kuwezesha majadiliano na watu binafsi au vikundi, inaweza kuchukua kati ya dakika 20-30, tafakari juu ya umuhimu wa kupata rasilimali na kuimarisha mifumo madhubuti ya kuzuia ukatili.

### Mwongozo wa majadiliano:

- Wakaribishe washiriki waangalie bango na washirikishane kuhusu muonekano wa bango na watafakari
- Wezesha mazungumzo kwa kuuliza maswali kama vile:
  - Je, jamii yako inawezaje kuhakikisha kwamba serikali zetu zinatimiza ahadi zao walizozitoa katika kutekeleza maazimio ya Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing?
  - Je, ni jitihada zipi unazoweza kuziunga mkono ili kuimarisha uwajibikaji katika kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake?
  - Je, ni ushirikiano wa aina gani unaoweza kuujenga ili kukusanya na kuimarisha rasilimali kwa ajili ya kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake?


Washukuru washiriki kwa muda wao waliotumia na wahimiza kushirikisha mawazo ya majadiliano kwa watu wengine.

Unaweza pia kubandika na kuonyesha bango lenye ukubwa wa A3 katika maeneo ya wazi yenye mkusanyiko wa watu wengi.

## 3. Kuwa mbunifu kwa kutengeneza bangili yako ya urafiki

Bangili ya urafiki inaashiria uhusiano na kujitoa, vinavyowakilisha uhusiano wa karibu katika kusaaidiana na uaminifu kati ya marafiki ambao wamejitolea kwaajili ya mabadiliko ya kijamii. Zinatumika kama ukumbusho dhahiri wa uzoefu wa pamoja na ahadi ya kusimama kwa pamoja, kuimarisha uhusiano wadhati na mshikamano.

Unapotengeneza bangili zako:

- Fikiria kuhusu dada/mwenzako ambaye anakutia moyo au anaye kuunga mkono, au kukuthamini. Unataka kuwaambia nini?
  - Je, kuna neno moja ambalo linawakilisha shukrani yako ambayo unaweza kuiweka kwenye bangili yako?
  - Unawezaje kusitawisha uhusiano mzuri ulio nao na wanaharakati wengine kwa kuwatia moyo na kuwathamini?
  - Je, juhudi zenye ushirikiano zinawezaje kuimarisha uwajibikaji na upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake?
- 
- 

#### 4. Tuungane kwa Kuvaa Utepe

Sambaza na uvae utepe mweupe au wazambarau, wenye ujumbe wa “Zuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.” Utepe huu unaashiria dhamira yako ya kutetea kuwepo kwa mifumo madhubuti ya uwajibikaji kwa ajili ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake, mipango iliyo na rasilimali za kutosha kwaajili ya kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake, na watunga sera kujitoa kwa upya kutekeleza dira kabambe iliyoainishwa kwenye Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing. Ikiwezekana vaa utepe kwa siku zote 16, au angalau wakati wa shughuli muhimu kama vile maandamano ya jamii.

#### 5. Fuata Mwongozo wa Shughuli za Vyombo vya Habari

Tumia Mwongozo wa Shughuli za Vyombo vya Habari ili kupanua wigo wako wa kufikia na kuungana na wadau mbalimbali. Unajumuisha kiti ya mitandao ya kijamii ili kushirikishana ujumbe wa Siku 16 za Unaharakati kwenye majukwaa kama vile Facebook, Twitter, Instagram, na WhatsApp, pamoja na mapendekezo yanayohusu kuhusisha vyombo vya habari vya ndani ya nchi.

#### 6. Tengeneza Shughuli Mbadala

Jisikie huru kuandaa shughuli zinazolingana na mahitaji mahususi ya jamii yako. Baadhi ya mapendekezo ni pamoja na:

##### Watu Binafsi:

- Tafakari kuhusu uzoefu wako binafsi unaohusiana na uwajibikaji katika kushughulikia suala la Ukatili Dhidi ya Wanawake.
- Andaa kijarida chenye mawazo yako kuhusu ongezeko la rasilimali linavyoweza kuongeza ufanisi katika kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.
- Tetea kuwepo kwa mifumo thabiti ya usaidizi kwenye mtandao wako.
- Anzisha mazungumzo na wengine kwa kutumia kadi ya safina, kwa kutafakari juu ya urithi wa wanawake waanzilishi wa Ufeminist wa Kiafrika.



### Mashirika:

- Andaa mijadala kuhusu umuhimu wa kuhuisha mifumo ya uwajibikaji iliyo na rasilimali za kutosha katika mikakati ya kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.
- Tambua mapungufu ya rasilimali na pendekeze masuluhisho yanayoweza kutekelezeka katika uboreshaji.
- Shirikiana na mashirika mengine na ushirikishane nao kuhusu mbinu bora na rasilimali.
- Andaa sherehe ya uandishi wa postikadi ambayo unaweza kuandika postikadi binafsi za wadau wakuu, kama vile wanaharakati wengine, mashirika, na watunga sera mapendekezo ya namna ya kuhamasisha utekelezaji wa ahidi walizozitoa kwenye Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing.
- Tambua majukwaa mbalimbali au fursa unazoweza kutengeneza za kushirikishana hadithi na kuendeleza majadiliano

### Jamii:

- Andaa warsha za kuelimisha wanajamii kuhusu Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing
- Anzisha mazungumzo kuhusu sera za ndani na ufanisi wake katika kusaidia usalama na ustawi wa wanawake.
- Imarisha ushiriki wa jamii ili kusaidia jitihada za uwajibikaji katika kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.
- Wezesha majadilino kwa njia ya bango lililopo kwenye kiti yako, hama-sisha mijadala mubashara kuhusu jinsi tunavyoweza kwa pamoja ku-komesha Ukatili Dhidi ya Wanawake kwa kutekeleza maono ya Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing.